Somola pili SHERIA NA INJILI (Law and Gospel)

Sisi kama walutherani tunahusika sana kulitumia neon la mungu kwa usahihi. “Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na mungu, mtendakazi asiye na sababu ya kutahayari, ukilitumia neon la kweli kuahalali. (2tim 2:15). Sehemu ya kushika vyema neon la mungu kwa kutunia mafundisho mawili ya Biblia kusahihi. Lini, jinsi gani na kwa nini tunatumia sheria na injili?

, MAANA NA KUPAMBANUA

Katika wimbo mmoja wa Isaac. Watts mafundisho haya mawili yalitofautishwa kwa usahihi.

- Sheria huamuru na hutufanya tujue ni majukumu gani tunawiwa au kupaswa kwa Mungu.

- Lakini injili hii lazima iwekwe wazi mahali hudanganya kwa nguvu zetu kufanya mapenzi yake.

- Sheria hufunua hatia ya dhambi na huonyesha mioyo yetu ilivyo

- Injili tu yaweza kueleza msamaha wa upendo na neema isafishayo.

- Laana hufanya sheria kushutunu baina ya mtu kwamba huanguka lakini mara moja.

- Lakini katika injili kristo hujitokeza kuondoa hatia ya miaka nyingi?

- Roho yangu usijaribu kuvuta maisha yake na faraja kutoka kwa sheria.

- Dunia katika tumaini linatokana na injili mtu anayetumaini ahadi huishi wimbo huu hutukumbusha kuwa injili ni habari njema ya Yesu mwokozi na kufa kwa ajili yetu, anaishi maisha makamilifu na kamwe hatungeweza na hata kufa kifo cha sadaka kubeba adhabu yetu, hivyo basi kupitia imani katika yeye kuwa na uzima wa milele. Kwa namna nyingine sheria hutubu kama wenye dhambi kutuonyesha mapenzi ya Mungu yalivyo na kwamba hatuwezi kuikamilisha katika maisha yetu. Mungu wetu ni Mtakatifu na mwenye haki agano la kale linatuambia na katika agano jipya linarudia. Basi ninyi mtakuwa watakatifu kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu (matt 5:48, law 19:2). Yesu wetu ni mwana kondoo mkamilifu wa mungu ambaye huondoa dhambi za ulimwengu kama mbatizaji alivyosema.....

Ghafla kama ukiuliza watu wengi jinsi gani waliokolewa, kama waliokolewa kwa kuzitii amri kumi watakuwa ni wengi ambao wangeweza kukubaliana nalo. Muonekano huo hufanya sheria kuwa sikitu na kumshusha Yesu kama mtu mwema kama mfano kwa watu.

LENGO

Lengo la sheria na injili lazima liwe limetunzwa kiusahihi, kushikilia neno la Mungu kikamilifu. Injili ni nguvu ya Mungu kwa wokovu Rum 1:16, Yoh 3:16, sambamba na vifungu vingi vituelezavyo kwamba wokovu ulikuwa umepatikana mlimani calvari na wala sio juu ya mlima Sinai.

Wokovu hauwezekani kuwa kwa sheria kama vifungu vifuatavyo visemavyo:-…… roho itendayo dhambi ndiyo itakayokufa” (Ez 18:4) “ maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote lakini akajikwaa katika moja amekosa juu ya yote. (Yakobo 2:10).

“kwa maana wale wote walio wa matendo ya sheria, walio chini ya laana maana limeandikwa, amelaaniwa kila mtu asiyedumu katika yote yaliyoandikwa katika kitabu cha Torati, asiyafunye. (Gal 3:10). Madhumuni makuu ya sheria ni kama kioo kutuonyesah hali yetu ya kupotea ….. kupitia sheria huja ufahamu wa dhambi (Rum 3:20). Hii humaanisha kwa watu wote wanaoangalia hitaji lao kubwa la mwokozi sheria pia ni kama kiongozi kwa wakristo kwamba wangeweza kuona kiusahihi katika neno la Mungu jinsi mapenzi ya Mungu yalivyo kwa maisha yao (Zab 119:105, 32). Pia inaweza kutumika kama kizuio kwa kutunza mlipuko hafifu wa dhambi katika dunia kwa ishara zake (zab 119:120, iim 1:9-10).

NGUVU.

Nguvu ipo katika injili na siyo katika sheria kuokoa kama tulivyoona katika Rum 1:16 na vifungu vingine. Mchungaji kurth hutupa mfano ili kuelezea hili. “Bwana mmoja alimwambia kijana wake, “kata na kupasuapasua kuni hizi leo. Kama hatafanya nitakuadhibu wakati nikifika nyumbani jioni. “ kijana yule

akajaribu lakini alikuwa dhaifu sana, hakuwa imara sana. Punde akaja kaka yake mkubwa na kusema, “kaa kando, nitafanya kwa ajili yako na alifanya sasa wakati babaye akija nyumbani atamwadhibu mtoto wake? Hapana, kama agizo (amri) lilitumwa, ingawa, kupitia mwingine lilitunzwa. Hivyo baba yetu wa mbinguni hutuambia nitafanya ……. Na hakufanya” tunajaribu lakini tu dhaifu na duni kwa mwili wa dhambi. Hivyo akaja kaka yetu mkubwa Yesu kristo na kusema, nitafanya kwa ajili yenu na aliweza, sasa wakati siku ikiwatimia, Mungu anaweza kutuadhibu? Hapana, sheria ilikuzwa, hasa kupitia mwingine (Yesu). Hivyo basi tunaokolewa na kristo katika sehemu yetu ambaye alitunza sheria kikamilifu kwa ajili yetu. Wema wake ni kwenda juu yetu kama vazi jeupe.

MSUKUMO

Msukumo wa maisha ya mkristo pia ni katika kutoka kwa injili. “kwa upendo wa Kristo watubidisha, kwa sababu tunadhibitisha mmoja alikufa kwa ajili ya wote, ili walio hai wasiwe hai tena kwa ajili ya nafasi zao wenyewe, hali kwa ajili yake yeye aliyekufa na akafufuka kwa ajili yao (2 Kor 5:14). Hatutafuti kufanya mema ili tuwe na dhawabu lakini kutafuta kutenda mema kwa kuwa kristo alikufa kwa ajili yetu na alienda kutuandalia makao ili alipo nasi tuwepo. Haitupaswi kuwa na hofu ya dhawabu, kwa sababu kristo amekwisha adhibiwa kwa ajili yeu. “katika upendo hauna hofu, lakini pendo lililo kamili huitupa nje hofu. (I Yoh 4:18).

MATOKEO

Katika luka 2:10-20 tunaona bila kuchelewa tokeo la kusikia injili ni furaha. Katika (lk 18:13) tunaona tokeo la sheria ni kuwa juu ya dhambi. Tunataka kuzungumzia pamoja sheria na injili. ”huzuni ya kimungu hufanya toba liletalo wokovu (IIYoh 7:10).

Katika maandishi ya akiri wa kilitheni katika muundo wa mapatano juu ya toleo hili tunakiri, tunaamini, kufundisha na kuungama kwamba ingawa mtu hlisi kuamini (katika Kristo) na ambaye Mungu kweli alimbadilisha kupitia Kristo kutoka kwa laana na shrutisho la sheria. Hawapo juu ya hesabu ila bila sheria, katika kutofautisha kabisa, wamekombolewa na mwana wa Mungu kwa usahihi kwamba wajidhibitishe wenyewe mchana na usiku katika sheria ……. Ingawa wamezaliwa mara ya pili hasa na wamefanywa upya katika roho na ufahamu zao, kama ufufuo na kufanywa upya haijakamilika katika ulimwengu huu. Kweli umeanza tu. Ni muhimu kwa sheria ya Mungu hasa kumulika njia zao ……. Muamini bila lazimisho au shurutisho lolote na kwa roho ya hiari sawa sawa na alivyozaliwa upya, kwa kutofanya makatazo ya sheria yangeweza kumsongonyoa milele kutoka kwake.

Kwa mwendo wa maisha yetu tunatafuta kushikilia neno la Mungu kiusahihi katika maisha yetu ya kila siku. Ni kielelezo kwamba tunatenda kiusahihi ndani yake. Ashukuriwe Mungu kwamba Roho wake hutenda kazi pamoja na roho zetu. Yesu ameahidi kwamba Roho wa kweli angetuongoza katika kweli yote, kuleta katika kumbukumbu zetu kile ambacho Yesu alisema, hutufundisha yote, na zaidi katika yeye tunaongea na kufundisha. Kwa Mungu wetu pekee huenda utukufu kwa neno lake kwetu na msaada wake kwetu kulitumia kiusahihi Amen.